# الأُضْحِيَّةُ

# فَضَائِلُهَا وَأَحْكَامُهَا

# UDH-HIYA

# FADHILA ZAKE NA HUKUMU ZAKE

Amesema Ibn Taymiyya رَحِمَهُ اللَّهُ: [Ama Udh-hiya, kauli iliyo dhahiri ni wajibu vilevile, kwa sababu hiyo (Udh-hiya) ni miongoni mwa alama kubwa za Uislamu na ni ibada yenye kuenea miji yote, na pia imefungamanishwa pamoja na swala…, nayo ni katika Mila (Dini) ya Nabii Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَامُ ambayo tumeamrishwa sisi kufuata mila yake][(1)].

Na amesema Ibn Uthaymin رَحِمَهُ اللَّهُ: [Kauli ya uwajibu ina nguvu zaidi kuliko kauli ya kupinga uwajibu (wa Udh-hiya), lakini kwa sharti kuwa na uwezo…][(2)].

---

[1]- Kitabu: [Majmuul fataawa] (Jz. 23, Uk. 162).
[2]-Kitabu: [As Sharhul mumtii'] (Jz. 7, Uk. 422).

بسم الله الرحمن الرحيم

# KIPAMBANUZI CHA KWANZA

## Maana ya neno Udh-hiya na hukumu yake:

Amesema Khatib As sharbiini (Allaah amrehemu):

"وَهِيَ مَا يُذْبَحُ مِنْ النَّعَمِ تَقَرُّبًا إلَى اللَّهِ تَعَالَى مِنْ يَوْمِ الْعِيدِ إلَى آخِرِ أَيَّامِ التَّشْرِيقِ"

**"Udh-hiya ni mnyama miongoni mwa wanyama hoa (ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo) anaye chinjwa katika siku ya Eid mpaka mwisho wa siku za tashriiq[(3)]) kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allaah"[(4)].**

Ibada hii imethibiti katika Qur'an, Sunna na Makubaliano ya waislamu. Allaah anasema:

﴿وَلِكُلِّ أُمَّةٖ جَعَلۡنَا مَنسَكٗا لِّيَذۡكُرُواْ ٱسۡمَ ٱللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلۡأَنۡعَٰمِۗ فَإِلَٰهُكُمۡ إِلَٰهٞ وَٰحِدٞ فَلَهُۥٓ أَسۡلِمُواْۗ﴾

**"Na kila umma tumewafanyia mahala pa kuchinjia (mihanga ya ibada) ili walitaje jina la Allaah juu ya vile alivyo waruzuku katika wanyama hoa. Basi Muabudiwa wenu mmoja tu, na kwake tu jisalimisheni"[(5)].**

Amesema sheikh Ibn Uthaymin رَحِمَهُ اللهُ: **[Aya hii inajulisha kwamba kila umma umewekewa sheria ya kuchinja kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allaah, na ni hoja ya wazi juu ya kwamba jambo hilo ni ibada yenye maslahi katika kila zama, sehemu na kila umma][(6)].**

Ama katika sunna imethibiti ibada hiyo kwa kauli, kitendo na kukiri kwake Mtume ﷺ:

---

[3]- Siku tatu zinazofuatia siku ya Eid (tarehe 11,12 na 13). zimeitwa hivyo kwa sababu ni siku za kuanika nyama, na hizi pia ni siku tukufu ambazo inapendekezwa kwa muislamu kukithirisha kuomba dua ndani yake: ربنا آتنا في الدنيا حسنة وفي الآخرة حسنة وقنا عذاب النار

[4]- Kitabu: [Mughnil muhtaaj] (Jz. 6, Uk. 122).

[5]- Surat Al-Hajj/34.

[6]- Ahkaamul udh-hiya (Uk. 5).

**Kauli yake:** Amesema Mtume ﷺ:

«مَنْ ذَبَحَ بَعْدَ الصَّلَاةِ تَمَّ نُسُكُهُ، وَأَصَابَ سُنَّةَ الْمُسْلِمِينَ»

**"Atakaye chinja baada ya swala imetimia ibada yake, na amepatia njia ya waislamu"(7).**

**Ama kitendo chake:** Amesema Anas ﵁:

«ضَحَّى النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِكَبْشَيْنِ أَمْلَحَيْنِ، فَرَأَيْتُهُ وَاضِعًا قَدَمَهُ عَلَى صِفَاحِهِمَا، يُسَمِّي وَيُكَبِّرُ، فَذَبَحَهُمَا بِيَدِهِ»

**"Mtume ﷺ alichinja kondoo wawili weupe sana, nikamuona ameuweka mguu wake ubavuni mwa shingo zao, (akawa) analitaja jina la Allaah (Bismillaahi) na anapiga takbira (Allaahu akbar), akawachinja kwa mkono wake"(8).**

Ama kukiri kwake: Amesema Jundub Bin Sufyan ﵁: **"Niliswali Eid al adh-ha pamoja na Mtume ﷺ, wakati alipomaliza kuwaswalisha watu, aliwaona mbuzi na kondoo wamechinjwa (kabla ya swala), akasema:**

«مَنْ ذَبَحَ قَبْلَ الصَّلَاةِ، فَلْيَذْبَحْ شَاةً مَكَانَهَا، وَمَنْ لَمْ يَكُنْ ذَبَحَ، فَلْيَذْبَحْ عَلَى اسْمِ اللهِ»

**"Aliyechinja kabla ya swala basi na achinje badala yake mbuzi mwingine, na yule ambaye hajachinja basi achinje kwa (kutamka) jina la Allaah"(9).**

Na wamekubaliana waislamu wote kwamba Udh-hiya ni miongoni mwa mambo yaliyomo ndani ya sheria ya kiislamu.

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ الله:

«وَلَا خِلَافَ فِي كَوْنِهَا مِنْ شَرَائِعِ الدِّينِ»

**"Na wala hapana khilafu yoyote kwamba Udh-hiya ni katika za sheria za dini hii"(10).**

---

7- Bukhari (5545) na Muslim (1961).
8- Bukhari (5558) na Muslim (1966).
9- Bukhari (5500) na Muslim (1960).
10- Fat'hul baari (Jz. 10, Uk. 3).

## Hukumu ya Udh-hiya:

Maulamaa wametafautiana kuhusiana na hukumu yake, je ni wajibu au sunna iliyo kokotezwa? Lakini amesema Ibn Taymiyya رَحِمَهُ الله hali ya kutilia nguvu upande wa uwajibu:

«وَأَمَّا الْأُضْحِيَّةُ فَالْأَظْهَرُ وُجُوبُهَا أَيْضًا فَإِنَّهَا مِنْ أَعْظَمِ شَعَائِرِ الْإِسْلَامِ وَهِيَ النُّسُكُ الْعَامُّ فِي جَمِيعِ الْأَمْصَارِ وَالنُّسُكُ مَقْرُونٌ بِالصَّلَاةِ.... وَهِيَ مِنْ مِلَّةِ إبْرَاهِيمَ الَّذِي أُمِرْنَا بِاتِّبَاعِ مِلَّتِهِ»

**"Ama Udh-hiya, kauli iliyo dhahiri ni wajibu vilevile, kwa sababu hiyo (Udh-hiya) ni miongoni mwa alama kubwa za Uislamu na ni ibada yenye kuenea miji yote, na pia imefungamanishwa pamoja na swala…, nayo ni katika Mila (Dini) ya Nabii Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَامُ ambayo tumeamrishwa sisi kufuata mila yake"**[11].

Ndiyo maana sheikh Ibn Uthaymin رَحِمَهُ الله baada ya kutaja hoja za pande zote mbili na pia kunukuu maneno hayo ya Ibn Taymiyya رَحِمَهُ الله akasema: **[Na kujiondoa kwenye shaka ni kwamba (mtu) mwenye uwezo asiche kuchinja, kwa sababu ya yale yaliyomo ndani yake ambayo ni kumtukuza Allaah na (kutukuza) utajo wake, na pia kujiondoa katika dhima kwa kufanya jambo lenye yakini]**[12].

---

[11]- Kitabu: [Majmuul fataawa] (Jz. 23, Uk. 162).

[12]- Kitabu: [Ahkaamul udh-hiya] (Uk. 14).

## KIPAMBANUZI CHA PILI

### Muda wa kuchinja Udh-hiya:

Ibada hii ya kuchinja ni ibada iliyowekewa wakati maalumu, haifai kutanguliza wala kuchelewesha, isipokuwa kuchelewesha kwa udhuru wa kisheria.

Mwanzo wa wakati wa kuchinja ni baada tu ya kumalizika swala ya Eid kwa wale walio katika miji, na wale walio mashambani au wasafiri watakadiria muda wa kuswaliwa swala ya Eid, na iliyo bora ni kuwa mtu asichinje isipokuwa baada ya kukamilika hotuba ya Eid, kwa sababu ndiyo mwenendo wa Mtume ﷺ, na endapo imamu amekuja na mnyama katika viwanja vya Eid basi asichinje mtu yeyote isipokuwa baada ya kuchinja imamu wake (kama alivyofanya Mtume ﷺ).

Na yeyote atakayechinja kabla ya swala amekosea na wala hatazingatiwa mnyama huyo kuwa ni Udh-hiya na badala yake anatakiwa achinje mnyama mwingine badala yake, kwa hadithi inayosema:

«مَنْ ذَبَحَ قَبْلَ الصَّلاَةِ فَلْيَذْبَحْ مَكَانَهَا أُخْرَى»

**"Aliyechinja kabla ya swala basi na achinje badali yake mnyama mwingine"[13].**

Na mwisho wa muda wa kuchinja ni baada ya kuzama kwa jua siku ya mwisho katika siku za Tashriiq (siku za Tashriiq ni tarehe 11, 12 na 13 dhul-hijja), kwa hiyo siku za kuchinja ni nne, kuanzia tarehe 10 ambayo ni siku ya Eid na siku tatu baada yake na hii ndio kauli yenye nguvu miongoni mwa kauli za maulamaa, na inafaa kuchinja wakati wa usiku lakini mchana ni bora zaidi, na mwisho wake ni siku 13 baada ya alasiri kabla ya kuzama jua.

[13]- Bukhari (5500) na Muslim (1960).

## KIPAMBANUZI CHA TATU

### Mnyama anayefaa kuchinjwa kwa ajili ya Udh-hiya:

Aina ya mnyama anayetakiwa kuchinjwa ni Ngamia, Ng'ombe, na Mbuzi au Kondoo, kwa kauli yake Allaah:

﴿وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنسَكًا لِّيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ﴾

**"Na kila umma tumewafanyia mahala pa kuchinjia (mihanga ya ibada) ili walitaje jina la Allaah juu ya vile alivyo waruzuku katika wanyama hoa"(14).**

**Wanyama hoa ni:** Ngamia, Ng'ombe, Mbuzi au Kondoo, na aliye bora katika kila aina ni yule aliye mweupe, mnene, mwenye pembe kwa hadithi inayosema:

«وَضَحَّى بِالْمَدِينَةِ كَبْشَيْنِ أَمْلَحَيْنِ أَقْرَنَيْنِ»

**"(Mtume ﷺ) alichinja akiwa Madina mbuzi wawili weupe, wenye pembe"(15).**

Na aliye mkamilifu wa viungo na maumbile huyo ni bora zaidi, lakini inafaa pia kuchinja mnyama aliye hasiwa kwa mujibu wa hadithi:

«أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ضَحَّى بِكَبْشَيْنِ سَمِينَيْنِ عَظِيمَيْنِ أَمْلَحَيْنِ أَقْرَنَيْنِ مُوْجَيَيْنِ»

**"Mtume ﷺ alichinja kondoo wawili, wanene, wakubwa weupe, wenye pembe, walio hasiwa"(16).**

---

[14]- Surat Al-Hajj/34.

[15]- Bukhari (1712) na Muslim (1966).

[16]- Musnad Ahmad (25686).

### Mnyama anetosheleza kuchinja kwa mtu mmoja na familia yake:

Mbuzi au kondoo mmoja anatosheleza kwa mtu mmoja kuchinja kwa ajili yake, familia yake, na yeyote anayemtaka miongoni mwa waislamu, na ngamia au ng'ombe anatosheleza kwa watu saba[17] na familia zao, kwa hadithi ya Jabir رَضِيَ اللهُ عَنْهُ:

**«نَحَرْنَا مَعَ رَسُولِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَامَ الْحُدَيْبِيَةِ الْبَدَنَةَ عَنْ سَبْعَةٍ، وَالْبَقَرَةَ عَنْ سَبْعَةٍ»**

**"Tulichinja pamoja na Mtume ﷺ mwaka wa (sulhu ya) Hudaybiya, ngamia mmoja kwa (kushirikiana) watu saba, na ng'ombe mmoja watu saba"[18].**

Na hadithi nyingine:

**«فَأَمَرَنَا رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنْ نَشْتَرِكَ فِي الْإِبِلِ وَالْبَقَرِ، كُلُّ سَبْعَةٍ مِنَّا فِي بَدَنَةٍ»**

**Alituamrisha Mtume ﷺ kushirikiana katika ngamia na ngo'mbe, kila watu saba miongoni mwetu kwa ngamia mmoja"[19].**

Ifahamike kwamba mtu anapochinja mbuzi au kondoo atashirikiana na familia yake katika ujira tu, kwa hiyo haitafaa kwa watu wawili wanaomiliki mbuzi au kondoo mmoja kushirikiana kwa kuchinja mbuzi mmoja, kwa sababu mbuzi si mnyama anayefaa kushirikiana katika Udh-hiya. Ama ngamia na ng'ombe inafaa kushirikiana katika umiliki na ujira pia, watu waliochangia watazingatiwa katika umiliki na pia katika ujira.

Amesema imamu Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ :

**«وَالشَّاةُ عَنْ وَاحِدٍ فَقَطْ بَلْ لَوْ اشْتَرَكَ اثْنَانِ فِي شَاتَيْنِ فِي تَضْحِيَةٍ أَوْ هَدْيٍ لَمْ يَجُزْ»**

**"Na mbuzi mmoja anatosheleza kwa mtu mmoja tu, na lau walishirikiana watu wawili kwa kuchinja mbuzi wawili katika Udh-hiya au mnyama wa Hijja haitafaa"[20].[21]**

---

[17]- Inaruhusiwa kushirikiana watu saba katika kununua ngamia au ng'ombe kwa ajili ya Udh-hiya.
[18]- Muslim (1213).
[19]- Muslim (1318).
[20]- Kitabu: [Nihaayatul muhtaaj] (Jz. 8, Uk. 133).
[21]- Haifai kwa watu wawili kuchinja mbuzi wawili wa Udh-hiya kwa kushirikiana, kwa sababu mbuzi si mnyama anaefaa kushirikiana katika kuchinja kwa Udh-hiya wala mnyama wa Hijja.

# KIPAMBANUZI CHA NNE

## Masharti kwa mtu anayekusudia kuchinja pamoja na kubainisha kasoro kwa mnyama wa Udh-hiya:

Tumetangulia kusema kwamba kuchinja kwa ajili ya Eidul Adh-ha ni ibada na ni kujikurubisha kwa Allaah, kwa hiyo haitasihi ila kwa masharti mawili:

1. Ikhlaas, afanya kwa ajili ya Allaah, na wala asikusudie katika ibada yake hiyo kujionesha, kusifiwa, au chochote katika pato la duniani.

Allaah anasema:

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ﴾

**"Na hawakuamrishwa ila wamuabudu Allaah hali ya kumtakasia yeye Dini, wawe waongofu"[22].**

2. Kumuiga Mtume ﷺ; afanye kama vile ilivyowekwa bila kuongeza wala kupunguza chochote, kwa hadithi inayosema:

«مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ»

**"Mwenye kufanya amali yoyote ambayo hakuna juu yake mafundisho yetu, basi atarudishiwa (haikubaliwi)"[23].**

Na pia ni lazima mnyama huyo awe amekamilisha masharti na kuepukana na vizuizi vya kutofaa kuchinjwa kwake, na masharti yake yamegawika katika sehemu kuu tatu:

1. Kuhusu wakati wa kuchinja, na hili tumelifafanua hapo nyuma.
2. Kadhalika idadi ya watu wa kushirikiana, nalo pia tumeelezea.
3. Ama kuhusu mnyama anayechinjwa, hili ndilo ambalo linahitaji ufafanuzi, katika kubainisha masharti yake manne yanayopasa.

---

[22]- Suratul Bayyina/5.
[23]- Bukhari (7349) na Muslim (1718).

a) Awe ni myama wa halali, haifai mtu kuchinja mnyama ambaye si halali yake, kama vile mnyama aliyeibwa, kuporwa, au mnyama aliyewekwa rehani n.k, ila kwa idhini ya yule mwenye haki yake.

b) Awe ni mnyama aliyetajwa katika maandiko ya kisheria, ngamia, ng'ombe, mbuzi au kondoo.

c) Awe ametimiza miaka iliyotajwa, ngamia wa miaka mitano, ng'ombe wa miaka miwili, mbuzi wa mwaka mmoja au kondoo wa miezi sita.

d) Awe amesalimika na kasoro zenye kuzuia kufaa kwake, nazo ni zile zilizotajwa katika hadithi ya Al-Baraa Bin Aazib رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema: **Alisimama kwetu sisi Mtume ﷺ akasema:**

**«أَرْبَعٌ لاَ تَجُوزُ فِي الأَضَاحِيِّ، فَقَالَ: الْعَوْرَاءُ بَيِّنٌ عَوَرُهَا، وَالْمَرِيضَةُ بَيِّنٌ مَرَضُهَا، وَالْعَرْجَاءُ بَيِّنٌ ظَلْعُهَا، وَالْكَسِيرُ الَّتِي لاَ تَنْقَي»**

**"Wanyama aina nne hawafai (kuchinjwa) kwa ajili ya Udh-hiya, akasema: mwenye chongo chenye kubainika, mwenye maradhi yenye kubainika, mwenye ulemavu wenye kubainika, na yule ambaye amekauka ubongo"[24].**

Wanyama wenye kasoro ambazo zimetajwa kwenye hadithi hii hawafai kabisa kuchinjwa kwa ajili ya Udh-hiya, kwa hiyo muislamu wakati wa kununua mnyama kwa ya kuchinja amchunguze vizuri mnyama huyo.

Amesema Ibn Qudama رَحِمَهُ الله :

**«فَلَا نَعْلَمُ بَيْنَ أَهْلِ الْعِلْمِ خِلَافًا فِي أَنَّهَا تَمْنَعُ الْإِجْزَاءَ»**

**"Wala hatujui sisi khilafu yoyote baina ya Maulamaa kwamba (kasoro hizo) zinazuia (mnyama) kufaa (katika Udh-hiya)"[25].**

---

[24]- Sunan Abi Daud (2802).

[25]- Al-Mughni/(Jz. 9, Uk. 441). Hii ni ishara ya kwamba kuna itifaki ya maulamaa wote juu ya hilo

## Baadhi ya kasoro zenye kujumuishwa na hizo (nne):

1. Mnyama asiye Ona (kipofu).
2. Mnyama aliyekula sana mpaka akazidiwa (kuvimbirwa), lakini endapo ataharisha na ikabainika kwamba hana maradhi yoyote basi wakati huo atafaa kuchinjwa.
3. Mnyama aliyeshikwa na uchungu wa kuzaa.
4. Mnyama aliyepatwa na sababu zenye kupelekea kwenye kifo, kama kunyongwa, kupigwa, kuanguka (kutoka sehemu ya juu), kupigwa pembe, na aliyeliwa na mnyama mbwawe (mnyama mwenye kushambulia). Kwa sababu mnyama mwenye hali hii anastahiki zaidi kutofaa kuliko mwenye maradhi yenye kubainika.
5. Mnyama asiyeweza kutembea kwa ajili ya maradhi.
6. Mnyama aliyevunjika mguu.

Hizi ni kasoro kumi zenye kuzuia mnyama kutofaa kuchinjwa kwa ajili ya Udh-hiya, nne miongoni mwa hizo ni kutoka kwenye hadithi, na sita ni kwa kukisia juu ya kasoro hizo zilizotajwa katika hadithi.

# KIPAMBANUZI CHA TANO

## Kasoro ambazo ni karaha kwa mnyama wa Udh-hiya:

Katika kipambanuzi kilichopita tumetaja kasoro zenye kuzuia mnyama kufaa kuchinjwa kwa ajili ya Udh-hiya, na sasa tutaelezea kasoro ambazo ni karaha kwa mnyama huyo lakini akikosekana mwingine atafaa kuchinjwa pamoja na kasoro hizo, kama wanavyosema wanachuoni.

1. Mnyama ambaye imekatika, kuvunjika au kung’oka pembe yake, ama yule asiye na pembe kimaumbile huyo si karaha.
2. Mnyama aliyekatwa juu ya sikio lake kwa upana.

3. Mnyama aliyekatwa chini ya sikio lake kwa upana.
4. Mnyama aliyekatwa sikio lake kwa urefu.
5. Mnyama aliyetobolewa sikio lake.
6. Mnyama aliyekatwa sikio lake mpaka likadhiri tundu.
7. Mnyama ambaye imeng'oka pembe yake.

Kasoro hizi zimeitwa kuwa ni karaha tofauti na zile zilizotangulia, kwa sababu ukifuatilia utapata kwamba zile nne zilitajwa wakati Mtume ﷺ alipokuwa anajibu swali, kwa hiyo lau ingelikuwa kuna kasoro nyingine za kutofaa pia angezitaja, kuacha kwake kuzitaja ni ishara ya kwamba kasoro zilizotajwa kwenye hadithi nyingine hukumu yake ni karaha, hivi ndivyo wanavyoeleza Maulamaa wetu. Lakini endapo mtu amekosa mnyama mwingine aliye bora zaidi basi atamchinja huyo mwenye kasoro zilizotangulia kutajwa hapo juu.

Na hujumuishwa pamoja na kasoro hizo kasoro zifuatazo:

1. Mnyama aliyekatwa mkia, ama yule asiyekuwa nao tangu asili atafaa.
2. Kondoo aliyekatwa kalio lake lote au zaidi ya nusu hatofaa, lakini aliyekatwa sehemu ndogo ya kalio lake atafaa, na asiyekuwa nalo tangu asili yake huyo atafaa kuchinjwa bila karaha yoyote.
3. Mnyama ambaye amekatwa dhakari yake.
4. Mnyama ambaye yameng'oka baadhi ya meno yake, tafauti na yule ambaye baadhi ya meno yake hayakuota tangu asili yake.
5. Mnyama ambaye imekatwa sehemu katika chuchu zake, na kama ni maumbile yake basi hakuna shida.

Hizi ni kasoro ambazo zikipatikana kwa mnyama yoyote, ngamia, ng'ombe, au mbuzi na kondoo, itakuwa ni karaha kumchinja, lakini si haramu.

## KIPAMBANUZI CHA SITA

### Hukumu mbalimbali juu ya mnyama aliye ainishwa kwa ajili ya Udh-hiya:

Atalazimika mnyama kuwa ni wa Udh-hiya kwa mambo mawili:

1. Kutamka kwa kumkusudia kwamba mnyama huyo ni wa Udh-hiya, na kama unakusudia kutoa habari tu, mfano kusema: (mbuzi huyu nitamchinja siku ya Eid In Shaa Allaah), basi hapo haitalazimu bali una hiyari.
2. Au kumchinja kwa nia ya Udh-hiya, hata kama hakutamka hapo kabla kwamba mnyama huyo ni wa Udh-hiya.

Kwa hiyo mnyama ambaye ameainishwa kwa ajili ya Udh-hiya anafungamana na hukumu zifuatazo:

a) Haifai kuhamisha umiliki kwa njia yoyote ile, si kwa kuuza wala kutoa zawadi/hiba, n.k, isipokuwa akikusudia kumuuza ili kumpata mnyama mwingine aliye bora zaidi ya huyo.

Na kama mmiliki wake amefariki basi warithi wake hawana haki ya kutengua jambo hilo wala kubadilisha, lazima wamchinje kwa ajili ya Udh-hiya.

b) Haijuzu kwake kumtumia katika shughuli zake kama kulima, kumpanda, kumkama maziwa ambayo itakuwa ni sababu ya kudhoofika kwake au ana mtoto anaye hitajia kunyonya (mtoto ambaye pia ameanishwa katika Udh-hiya) n.k.

c) Endapo mnyama huyo atapata kasoro yoyote kama vile kuvunjika mguu n.k, na akawa yeye ndiye muhusika basi atamchinja mnyama mwingine kama huyo badali yake, lakini kama amepata kasoro mwenyewe tu, atafaa kuchinjwa na atakuwa ametosheleza.

Na kama ametiwa kasoro na mtu mwingine na akawa hana uwezo wa kulipa, basi atamchinja pamoja na kasoro yake hiyo, lakini kama ana uwezo basi anunue mnyama mwingine na ampatie yule mmiliki wa mnyama huyo kwa ajili ya kumchinja.

d) Endapo mnyama huyo ameibiwa au kupotea kwa uzembe wa mmiliki, basi atanunua mnyama mwingine mfano wake na atamchinja, lakini kama si kwa uzembe basi hakuna juu yake kulipa chochote, na akimpata au kumkamata yule aliyeiba, basi atamchinja mnyama huyo hata kama umepita muda wake wa kuchinja.

e) Mnyama aliye ainishwa kwa ajili ya Udh-hiya akizaa basi hukumu ya mwanawe ni sawa na hukumu yake, ni sawa mimba hiyo aliipata kabla au baada ya kuainishwa kwake.

f) Ikiwa kuna watu wawili kila mmoja amechinja mnyama wa mwenzie kimakosa na akawa ni mnyama huyo ameainishwa kwa ajili ya Udh-hiya basi itatosheleza, na kama hawakuafikiana katika kugawana nyama basi kila mmoja atamrejeshea mwenzie nyama yake ili aigawe mwenyewe.

## Je, mwanamke anafaa kuchinja na je kichinjwa chake ni halali?

Amesema Ibn Qudama (Allaah amrehemu):

**"قالَ ابْنُ الْمُنْذِرِ: أَجْمَعَ كُلُّ مَنْ نَحْفَظُ عَنْهُ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ، عَلَى إبَاحَةِ ذَبِيحَةِ الْمَرْأَةِ وَالصَّبِيِّ"**

**"Amesema Ibnul Mundhir: Wamekubaliana maulamaa wote ambao tumehifadhi kutoka kwao elimu, juu ya uhalali/kufaa kwa mnyama aliyechinjwa na mwanamke na mtoto mdogo (mwenye kupambanua)".** Na alipoitaja hadithi ya mjakazi (mtumwa wa kike) wa Kaab Bin Malik ambaye alichinja mbuzi katika zama za Mtume Swala na Salamu zimshukie) akasema:

**"وَفِي هَذَا الْحَدِيثِ فَوَائِدُ سَبْعٌ؛ أَحَدُهَا، إبَاحَةُ ذَبِيحَةِ الْمَرْأَةِ وَالثَّانِيَةُ، إبَاحَةُ ذَبِيحَةِ الْأَمَةِ. وَالثَّالِثَةُ إبَاحَةُ ذَبِيحَةِ الْحَائِضِ"**

**"Na kuna katika hadithi hii faida saba; ya kwanza, uhalali wa kichinjwa cha mwanamke, ya pili: uhalali ya kichinjwa cha mjakazi/mtumwa wa kike, ya tatu: uhalali wa kichinjwa cha mwanamke mwenye hedhi…"[26].**

[26]- Tazama: [Al-Mughni] (Jz. 9, Uk. 388).

## Kiwango cha kula na kugawa Udh-hiya:

Allaah Subhaanahu wata'alaa anasema:

﴿لِّيَشْهَدُوا۟ مَنَٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا۟ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ۖ فَكُلُوا۟ مِنْهَا وَأَطْعِمُوا۟ ٱلْبَآئِسَ ٱلْفَقِيرَ﴾

**"Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la Allaah katika siku maalumu juu ya wanyama hoa alio waruzuku. Basi kuleni katika hao na mlisheni mweye shida aliye fakiri mno"[27].**

Na Mtume ﷺ amesema:

«كُلُوا وَأَطْعِمُوا وَادَّخِرُوهَا»

**"Kuleni, mlisheni (masikini n.k), na itunzeni"[28].**

Ama tamko la imamu Muslim katika sahihi yake:

«فكُلُوا وَادَّخِرُوا وَتَصَدَّقُوا»

**"Kuleni, ihifadhini na toeni sadaka".**

Ukiangalia kwa mazingatio utapata kwamba tamko la imamu Bukhari رَحِمَهُ الله ni lenye kuenea zaidi kwa sababu tamko (it'aam - kulisha) ni lenye kuenea: kutoa sadaka kwa masikini, na pia kuwapatia matajiri kwa njia ya zawadi. Hakuna katika aya au hadithi zilizo tangulia ushahidi wowote kuhusiana na kiwango cha kula, kutoa sadaka kwa masikini au kutoa zawadi kwa matajiri, kwa hiyo jambo hilo ni lenye wasaa, mtu ataangalia hali na mazingira yake na mahali anapoishi, hata kama atakula nyama yote, basi hapana ubaya. Lakini baadhi ya wanachuoni wanaona kwamba theluthi moja atakula, nyingine atatoa sadaka na theluthi ya tatu ataihifadhi.

---

[27]- Suratul Hajj/28.
[28]- Bukhari (5556).

Na mtu aliyepewa sadaka ana haki ya kuiuza nyama hiyo au kuitumia katika matumizi mengine kwa sababu hiyo ni mali yake, na endapo ataiuza haifai kununua yule aliyempatia mwanzo ambaye ndiye mmiliki wa asili wa mnyama huyo.

## KIPAMBANUZI CHA NANE

### Mambo ya kujiepusha nayo mtu anaye kusudia kuchinja:

Imepokewa kutoka kwa Ummu Salama رَضِيَ اللهُ عَنْهَا , kwamba Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا رَأَيْتُمْ هِلَالَ ذِي الْحِجَّةِ، وَأَرَادَ أَحَدُكُمْ أَنْ يُضَحِّيَ، فَلْيُمْسِكْ عَنْ شَعْرِهِ وَأَظْفَارِهِ»

**"Mkiuona mwezi mwandamo wa Dhul-Hijjah (mfungo tatu) na mmoja wenu akakusudia kuchinja (Udh-hiya), basi ajizuie kunyoa nywele zake na kukata kucha zake"**[29].

Katika hadihti hii kuna katazo la kukata kucha au ngozi ya mwili wako kama ilivyokuja katika hadithi nyingine, na pia kunyoa nywele za aina zote katika mwili kwa mtu ambaye amekusudia kuchinja Udh-hiya, na endapo alikusudia kuchinja baada ya kupita siku kadhaa tangu kuandama kwa mwezi, na akawa tayari amekata kucha au kunyoa nywele zake basi hapana vibaya, atajizua kwa siku zilizobaki.

Amesema Sheikh Ibn Uthaimiin رَحِمَهُ الله: **[Maulamaa wametafautiana kuhusu katazo hili, je ni la uharamu au karaha? Lakini iliyo sawa ni kwamba ni katazo la uharamu, kwa sababu ndiyo asili katika katazo, na hakuna dalili yoyote yenye kuliepusha katazo hilo na uharamu, lakini hakuna fidia yoyote (kwa mwenye kufanya hivyo) kwa sababu ya kukosekana dalili juu ya hilo]**[30].

---

29- Muslim (1977).

30- Ahkaamul Udh-hiya wad-dhakaat (Uk. 53).

Wanachuoni wametafautiana kuhusiana na hekima ya katazo hilo, kuna waliosema kwamba mtu mwenye kuhirimia/kukusudia Hija au Umra haruhusiwi kunyoa nywele zake, basi vivyo hivyo mwenye kukusudia kuchinja asifanye hivyo ili kufanana na mwenye kuhirimia katika baadhi ya matendo ya ibada ya kuchinja, na wengine wametaja hekima nyigine. Wallaahu a’alam.

Kuna baadhi watu wanadhani kwamba mtu aliyetia nia ya kuchinja kisha akanyoa au kupunguza nywele zake, au akakata kucha au ngozi ya mwili wake hatakubaliwa kuchinja kwake, jambo hili si sahihi, lakini mwenye kufanya hivyo bila ya udhuru wowote wa kisheria atakuwa ametumbukia katika makatazo na kwenda kinyume na amri ya Mtume ﷺ, kwa hiyo itamlazimu kuleta Istighfaar na kumuomba Allaah toba.

Na katazo hili atahusika nalo mtu mwenye mnyama wa kuchinja wala mkewe, mtoto n.k pia hatahusika aliyopewa uwakala wa kusimamia mnyama wa mtu mwingine, hao wote wanaruhusiwa kunyoa nywele zao, kukata kucha n.k.

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

**Jumatatu 1/Dhul-Hijjah/1444H - 19/06/2023H**

**Pongwe-Tanga**

**Tanzania.**